Candidate's Number _____

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF [illegible]

Nambari ya Mtahiniwa _____

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION AND CULTURE
FORM TWO SECONDARY EDUCATION EXAMINATION, 1992

0011 ELIMU YA SIASA

MUDA: Saa 2

Jibu maswali yote katika karatasi hii na andika namba yako ya mtihani kila ukurasa.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU

| SWALI | ALAMA | SAHIHI |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| JUMLA | | |

Karatasi hii ina kurasa 4 zenye maandishi.

B. Waingereza

Nambari ya Mtahiniwa _____

## SEHEMU A

Soma habari ifuatayo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.

Muundo wa uongozi ni mgawanyo wa madaraka katika ngazi mbalimbali za jamii. Jamii za kale nazo zilikuwa na miundo yake ya uongozi. Miundo hiyo iliyofautiana kutokana na mila, desturi na ukubwa wa jamii. Katika miundo ya uongozi wa jadi, ngazi ya mwanzo kabisa ilikuwa familia. Katika ngazi hii viongozi wake walikuwa baba na mama. Wao ndiyo waliokuwa wakuu wa familia. Wajibu wao mkubwa ulikuwa kuzipatia familia zao mahitaji muhimu kama vile chakula, malazi, mavazi na malezi bora. Pia walipaswa kuhakikisha ulinzi na usalama wa familia zao.

Katika familia watoto wao walikuwa na wajibu wa kufuata maelekezo yaliyotolewa na wazazi wao, pia waliwajibika kuwatii na kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali kama vile za kuzalisha mali.

Ngazi iliyofuata ni ukoo. Familia za ukoo mmoja zilikuwa na kiongozi. Kiongozi wa ukoo alikuwa mzee au mtu mwenye sifa za uongozi bora. Kiongozi wa ukoo ndiye aliyekuwa akishughulikia mambo yote ya ukoo, na aliyeongoza shughuli zote za uzalishaji mali katika ukoo. Pia alikuwa kiongozi wa dini mwenye uwezo wa kutambikia mizimu.

Wakati mwingine koo mbalimbali ziliungana na kuwa jamii moja chini ya kiongozi mmoja aliyetambulika katika eneo kubwa. Viongozi wa jamii walijulikana kwa majina mbalimbali kutokana na lugha na mazingira ya jamii. Mfano wa majina hayo ni kama Mtwa (Uhehe), Mangi (Uchaga), Mtemi (Unyanyembe), Mndewa (Ukaguru), Zumbe (Uzigua). Katika ngazi hii ya uongozi, Kiongozi mkuu alikuwa yule wa jamii nzima na viongozi wa koo walikuwa chini yake. Viongozi wa jamii walitawala, walihukumu, walitambika na walifanya mambo mengi muhimu kwa niaba ya jamii nzima.

Maswali:

(a) Muundo wa uongozi wa jamii moja uliweza kutofautiana na muundo wa jamii nyingine. Taja vitu vitatu vilivyotofautisha miundo hiyo ya uongozi.

(b) Kwa kifupi eleza muundo wa uongozi ni nini?

(c) Majina ya viongozi wa jamii mbalimbali yalitokana na vitu viwili muhimu. Vitaje.

(d) Taja mojukumu matatu ya viongozi wa jamii.

(e) Unafikiri habari hii inazungumzia nini?

## SEHEMU B

2. (a) Katika harakati za mageuzi zinazoendelea, CCM imelazimika kufunga shughuli zake katika mkoa wake mmoja kichama. Mkoa huo ni _____.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION

FORM TWO SECONDARY EDUCATION EXAMINATION, 1969



Nambari ya Mtahiniwa _____

(b) Katika kuitikia matakwa ya mfumo wa vyama vingi vya siasa, CCM imelazimika kufunga aina moja ya matawi yake. Matawi hayo ni _____.

3. Wageni waliovamia nchi yetu na kuitawala kwa nyakati tofauti ni:

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

(iv) _____

4. Chama cha Mapinduzi kinaamini kwamba:

(i) _____

_____

(ii) _____

_____

(iii) _____

_____

5. Taja aina nne za Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano

(i) _____

_____

(ii) _____

_____

(iii) _____

_____

(iv) _____

_____

6. Mambo yaliyosaidia kufanikisha ukombozi wa kisiasa katika nchi yetu ni:

(a) _____

_____

(b) _____

_____

D. Waarabu ( )

Nambari ya Mtahiniwa _____

(c) _____

_____

(d) _____

_____

## SEHEMU C

7. Andika insha fupi ukieleza sababu za kuingia kwa wakoloni katika nchi yetu na njia au mbinu walizotumia kuingia nchini.

8. Eleza maana ya:

   (a) Wabunge wa taifa

   (b) Jinsi wanavyopatikana.

_____